Jamhuri ya
Muungano wa
Tanzania

No. xxxx/2024

Taarifa Fupi ya Kisera, 2020:

# UFANISI WA MIFUKO NA PROGRAMU ZA SERIKALI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZINAZOLENGA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI



Juni, 2024
Wizara ya Fedha

Taarifa Fupi ya Kisera, 2020:

# UFANISI WA MIFUKO NA PROGRAMU ZA SERIKALI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZINAZOLENGA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI

Wizara ya Fedha

# 1. Muhtasari

Chapisho hili linatoa matokeo ya utafiti wa ufanisi wa mifuko na programu za serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazolenga wajasiriamali wadogo na wa kati. Utafiti ulifanywa kubainisha mifuko na programu zilizopo, malengo yake, huduma zitolewazo na changamoto za kufikia malengo.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mifuko na programu zimeleta mafanikio mbalimbali kama kuwezesha upatikanaji wa huduma ya fedha jumuishi mfano mikopo ya riba na masharti nafuu ambayo imesaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kujikwamua kiuchumi ikiwemo kuanzisha biashara na kilimo na kumudu mahitahi mbalimbali (afya, kulipa ada za shule, ujenzi wa makazi na akiba). Utafiti pia ulibaini changamoto kadhaa zinazoikabili mifuko, programu na wajasiliamali ikiwa ni pamoja na uchelewaji wa mikopo, kushabihiana kwa majukumu kwa baadhi ya mifuko, uwepo wa mikopo chechefu, ukosefu wa mifumo ya ufuatiliaji mikopo, utegemezi kwa serikali kuu na mitaji midogo. Uwepo wa riba kubwa kwa baadhi ya mifuko, ukosefu wa taarifa na elimu na urasmu na uchelewaji wa mikopo ni baadhi ya changamoto zilizobainishwa kuwakabili wajasiliamali.

Uwepo wa riba kubwa kwa baadhi ya mifuko, ukosefu wa taarifa na elimu na urasmu na uchelewaji wa mikopo ni baadhi ya changamoto zilizobainishwa kuwakabili wajasiliamali.




Utafiti unapendekeza kuwa kuna umuhimu wa mifuko na programu kubuni vyanzo vingine endelevu vya fedha ili kuwezesha kufikia wanufaika wengi zaidi, kuweka masharti nafuu zaidi kuhusu dhamana, kupunguza riba za mikopo, kupunguza mlolongo na muda wa kutoa mikopo, kuwepo kwa mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia wakopaji pamoja na usimamizi wa marejesho ili kupunguza mikopo chechefu. Utafiti unapendekeza kuwa kuna haja ya kuunganisha baadhi ya mifuko na programu ambazo majukumu na wanufaika wake wanashabihiana ili kupunguza gharama za kuendesha na kuongeza ufanisi wa kuwahudumia wananchi.

# 2. Utangulizi

Upatikanaji wa mitaji ni moja ya nyenzo muhimu katika kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, wajasiriamali kutoka makundi haya kwa muda mrefu wameshindwa kupata mikopo katika taasisi za kibiashara kutokana na changamoto kubwa walizonazo ikiwemo kipato kidogo na kukosa dhamana za mikopo. Wajasiriamali wa makundi haya pia wamekuwa na changamoto za elimu na uelewa kuhusu mikopo na usimamizi wa biashara. Changamoto nyingine ni pamoja na kutokuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba; benki kutotoa mikopo yenye masharti nafuu; riba kubwa na tozo mbalimbali; ukosefu wa mikopo inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kukosekana kwa uwazi wa masharti ya mikataba ya mkopo; utoaji holela wa mikopo ambao unasababisha limbikizo la madeni kwa wateja na utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa madeni ambao unasababisha wananchi kupoteza mali zao.

Hivyo, ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi hasa wajasiriamali wadogo na wa kati wanafikiwa na kunufaika na mikopo Serikali ilianzisha mifuko na programu maalumu kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wajasilimali wadogo na wakati. Aidha, pamoja na uwepo wa mifuko na programu hizo za uwezeshaji wananchi kiuchumi, ilionekana kwamba bado hazijafikia malengo yaliyokusudiwa na hivyo utafiti huu ulilenga kupima ufanisi katika utendaji mifuko na programu za Serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi, kubainisha changamoto zinazowakabili wajasiriamali na wasimamizi wa mifuko na programu pamoja na kutoa mapendekezo ya namna bora ya uendeshaji, usimamizi na uendelevu wa mifuko na programu hizo.



utoaji holela wa mikopo ambao unasababisha limbikizo la madeni kwa wateja na utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa madeni ambao unasababisha wananchi kupoteza mali zao.

# 3. Mbinu za Utafiti

Utafiti ulitumia taarifa za msingi pamoja na marejeo. Taarifa za msingi zilikusanywa kupitia madodoso na mahojiano na wasimamizi na wanufaika wa mifuko na programu 24 za uwezeshaji wananchi kiuchumi mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja 11; mifuko inayotoa dhamana 9; na mifuko inayotoa ruzuku 4. Utafiti huu ulijumuisha wajasiriamali wanufaika 381 na wajasiriamali ambao wasio wanufaika 212 kutoka mikoamikoa 10 ya Tanzania Bara:, Pwani, Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Lindi, Tabora, Mwanza, Mbeya na Shinyanga. Uchaguzi wa mikoa hiyo ulizingatia hali ya upatikanaji wa huduma za fedha kwa wote ambapo mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Iringa, Mwanza na Pwani ilionekana kuwa na upatikanaji mkubwa, mikoa ya Mbeya, Shinyanga na Lindi ilikuwa na upatikanaji wa kati na mkoa wa Tabora ulikuwa na upatikanaji mdogo wa huduma za fedha. Uchaguzi wa mikoa pia ulilenga kuhakikisha sampuli jumuishi ya mikoa yenye upatikanaji mkubwa wa huduma na yenye upatikanaji mdogo pamoja na mgawanjiko wa kanda za kijografia. Taarifa za marejeo zilipatikana kwa kupitia sheria, kanuni, mikataba, miongozo pamoja na nyaraka mbalimbali za utendaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazowalenga wajasiriamali wadogo na wa kati.

# 4. Matokeo ya Utafiti


### Idadi ya Mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi

Utafiti ulibaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Serikali ilikuwa ina jumla ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 54. Hii inaonesha kwamba Serikali imewekeza nguvu katika kuhakikisha wajasiriamali wanapata mikopo kutoka kwenye Mifuko na Programu hizi ili kujiinua kiuchumi.

### Mgawanyo wa wanufaika

Matokeo yameonesha kuwa maeneo ya mijini yana wanufaika wengi wa mifuko na programu (71.9%) ikilinganishwa na maeneo ya vijijini (28.1%). Ufahamu wa wajasiriamali kuhusu Mifuko na Programu za Uwezeshaji wananchi kiuchumi: Utafiti umebaini kuwa wajasiriamali wengi hawana ufahamu wa mifuko yote inayohusu wajasiriamali wadodo na wa kati. Kati ya mifuko 54 iliyopo ni mifuko michache tu ndiyo inafahamika na wananchi wengi (**Kielelezo Na. 1**). Hii inaonesha kuwa kuna haja ya mifuko na Programu kujitangaza vyema ili ijulikane na kufikiwa na wajasiriamali wengi zaidi.

### Kielelezo Na. 1: Mifuko na Programu Zinazofahamika zaidi na Wananchi





### Mchango wa Mifuko na programu katika upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali

Matokeo ya utafiti yalionesha kuwa wajasiriamali wengi wanapata mitaji kutoka sekta za kifedha zisizo rasmi kama vile:

- Akiba (68.6%)
- Msaada (13.1%)

Aidha, huduma ndogo za fedha ,vikundi vya kijamii na SACCOS zilionekana kuwa na mchango mdogo katika kutoa mitaji kwa wajasiriamali (Kielelezo Na. 2). Hii inaonyesha kwamba licha ya uwepo wa sekta rasmi za fedha mwamko bado ni mdogo katika kupata mitaji kupitia sekta hizo.

### Kielelezo Na. 2: Vyanzo vya Mtaji kwa Wajasiriamali wa Mifuko na Programu




Kuna haja ya mifuko na Programu kujitangaza vyema ili ijulikane na kufikiwa na wajasiriamali wengi zaidi.

### Mchango wa mifuko na programu katika kuongeza wigo na kukuza ajira

Utafiti ulibaini kuwa Mifuko na Programu zimesaidia kutengeneza ajira kwa watu wengine ambao sio wanufaika wa moja kwa mpoja wa mikopo hiyo. Mfano, kwa wanufaika wote waliohojiwa waliweza kuajiri jumla ya wafanyakazi 4,325 baada ya wanufaika kupata mikopo, sawa na wastani wa watu 11 kwa kila mnufaika. Hii inaonesha kuwa Mifuko na Programu ni chanzo kikubwa cha ajira katika jasiriamali ndogo na za kati.

> Kwa wanufaika wote waliohojiwa waliweza kuajiri jumla ya wafanyakazi 4,325 baada ya wanufaika kupata mikopo, sawa na wastani wa watu 11 kwa kila mnufaik


### Changamoto zinazowakabili waendeshaji na wasimamizi wa mifuko na Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi

- Muda wa kuomba hadi kupata mkopo
- Kushabihiana kwa majukumu kwa baadhi ya mifuko
- Uwepo wa mikopo chechefu
- Ukosefu wa mfumo wa pamoja wa ufuatiliaji wa mikopo
- Mitaji midogo ikilinganishwa na mahitaji
- Ukosefu wa watendaji wa moja kwa moja katika ngazi ya halmashauri
- Utegemezi mkubwa kwa serikali kwenye mtaji na gharama za uendeshaji wa mifuko na programu

### Changamoto zinazowakabili wajasiriamali katika kupata huduma kwenye Mifuko na Programu

- uwepo wa riba kubwa kwa baadhi ya mifuko (37%), ya 17% mpaka 22%.
- kukosa taarifa na elimu ya mikopo na ujasiriamali (21%),
- uaminifu na ushirikiano (11%),
- urasimu katika upatikanaji wa mikopo (7%),
- udogo wa mikopo inayotolewa na Ucheleweshaji wa utoaji wa mikopo (7%).

**Kielelezo Na. 3: Changamoto zinazowakabili wajasiriamali wa Mifuko na Programu**



# 5. Hitimisho na Mapendekezo

Utafiti huu umeonyesha kuwa Mifuko na programu za Serikali zinazowawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati kwa ujumla zimeonesha kuwanufaisha wajasiriamali walio wengi na uchumi wa nchi kwa ujumla. Utafiti pia umebaini changamoto mbalimbali zinazokabili mifuko, programu na wajasiliamali wa kati na chini. Hivyo, mifuko na programu iweke jitihada katika kushughulikia changamoto hizi ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kunufaika. Aidha, utafiti huu umeainisha maeneo ya kisera na usimamizi ya kuboresho ufanisi katika uendeshaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

» Kuanzishwa kitengo maalumu katika ngazi ya Wizara Mikoa na Halmashauri kwa ajili ya usimamizi wa mikopo inayotolewa ili kuwezesha usimamizi katika ngazi ya chini;

» Mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ziwe na mifumo thabiti ya kielektroniki kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini;

» Kuhakikisha tathmini ya biashara au mradi wa kila maombi ya mkopo ili kuhakikisha mikopo inatolewa kwa biashara na miradi inayotekelezeka na kuepusha mikopo chechefu;

» Kuimarisha elimu na mafunzo kuhusu sheria na kanuni za usimamizi na uendeshaji wa mifuko na programu kwa watendaji wanaosimamia mifuko/programu;

» Wanufaika wa TASAF wafanyiwe tathimini ili kubaini kaya maskini zilizofuzu ili kuziondoa kwenye mpango na kuwezesha Serikali kuwahudumia wengine wenye uhitaji;

» Mifuko iongeze kutoa elimu na mafunzo ya uandaaji wa maandiko ya miradi, usimamizi wa biashara na usimamizi wa mikopo ili waweze kuendeleza biashara na kufanya urejeshaji wa mikopo kwa wakati;

» Mifuko iongeze kujitangaza na kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi ili walengwa waweze kuifahamu na kunufaika;

» Mifuko na programu ziweke utaratibu wa kuwafuatilia wajasiriamali wadogo na wa kati ili kufahamu changamoto na mwenendo wa shughuli/biashara na kuona namna ya kuwasaidia;

» Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa urasimishaji wa ardhi na makazi kwa kuwezesha upatikanaji wa hati kwa ajili ya dhamana za mikopo; na

» Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha mifuko na programu ambazo malengo na wanufaika wake wanashabihiana ili kupunguza mzingo wa usimamizi na kuongeza ufanisi.

» Mifuko na Programu iwekeze nguvu katika kufikia vijana wengi ili waweze kujiajiri kwa kupitia mikopo inayotolewa kwakuwa nguvu kazi kubwa ya Taifa iko kwa vijana.
kwa vijana.

Wizara ya fedha
Mji wa Serikali
Mtaa wa Hazina
Dodoma
http://www.mof.go.tz